

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

WEWE MTU MWONGO, TAHADHARI

*Hadithi hii imenakiliwa kutoka
kisa cha Matendo 5:1-11*

Baada ya siku ya Pentekoste wengi wa Wakristo hao wapya walianza kuuza manyumba na mashamba zao na kuleta pesa walizopata kwa mitume “kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji” (Matendo 4:35). Kwa muda mfupi watakatifu hao wa Yerusalemu walishiriki kila kitu kwa pamoja huku wakifanya ushirika wa kila siku na kuendelea katika mafundisho ya mitume. Lakini jambo hili halikuendelea Yerusalemu kwa muda mrefu, na pia halikuenea mahali kwingine. Pia haikuwa lazima kwa Wakristo hao wa Yerusalemu kuuza mali yao, bali lilikuwa tendo la kujitolea kwa jumuiya yao ya imani na ushirika huo wao.

Hebu tafakari kuhusu Wakristo hao ambao walikuwa na furaha kubwa katika imani yao huku wakileta pesa zao kwa mitume kutokana na mauzo ya mali yao ya kidunia. Fikra zao zilikuwa kwa mambo ya mbinguni, na walikuwa “wakiuza kila kitu” ili kujiandaa kwa ajili ya kurudi kwa Yesu Kristo. Katika kipindi hiki ambacho Wakristo hao walikuwa wakifanya sadaka maalum kama hiyo, mume mmoja na mkewe waliojulikana kama Anania na Safira waliuza shamba lao. Lakini kinyume na wale wengine ambao walikuwa wakiuza mali yao kwa furaha na kupatia kanisa mapato yao yote, Anania na Safira walijadili kati yao na kuamua kujiwekea kiasi fulani cha fedha ambazo walikuwa wamepata. Ukweli ni kwamba, hizi zilikuwa pesa zao, na hawakuwa na jukumu la kutoa hata shilingi moja; lakini kwa pamoja wakaamua kujifanya kwamba sadaka hiyo yao ilikuwa ya pesa zote ambazo walikuwa wamepata.

Huenda Anania aliingia mahali hapo watakatifu walikuwa wakifanya mikutano huku akiwa na

tabasamu la kutoka sikio moja hadi lingine, na kuanza kuwaambia wenzake jinsi alikuwa ameuza mali yake na sasa anazitoa pesa zote kwa kanisa. Kwa kiburi na “unyenyekevu” usio wa kweli, Anania aliwapatia mitume pesa hizo. Lakini mtume Petro, huku akijua kilichokuwa kikiendelea, akamuuliza, “Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja? Kilipokuwa kwako, hakikuwa mali yako? Na kilipokuwa kimekwisha kuuzwa, thamani yake haikuwa katika uwezo wako? Ilikuwaje hata ukaweka neno hili moyoni mwako? Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu.”

Mara moja Anania akaanguka chini akafa. Siku haikufika mwisho kama ambavyo Anania alitarajia; maisha yake ya milele yakaanza papo hapo huku moyo mwake ukiwa katika hali ya dhambi na unafiki. Haikuwa lazima kwa Anania kulipatia kanisa chochote kile. Hata angetoa asilimia ishirini na kubakisha fedha zingine. Dhambi yake ilikuwa kusema uongo. Yeye alisema jambo ambalo halikuwa la kweli kwa kujaribu kuwahadaa wenzake ili wafikiri kwamba alikuwa akitoa asilimia mia moja ya alichopata katika mauzo hayo. Lakini kulingana na Petro, dhambi kubwa zaidi ya Anania ilikuwa kwamba yeye alikuwa amemdanganya Mungu moyoni make. Mbele ya uwepo mwake Mungu na mwanadamu, dhambi ya Anania ya kusema uwongo na kuhadaa wenzake ikawekwa wazi, naye Mungu akamhukumu kufa.

Hofu kuu ikatanda kwa kila mtu ambaye alikuwa ameshuhudia au kusikia jambo hilo. Hukumu kali ya Mungu dhidi ya dhambi ya udanganyifu na unafiki ikajulikana kwa watu wote. Huku watu wakiwa wamepigwa na

(Endelea katika Ukurasa 2)



“Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu...? Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu.”

Tahariri

3

Mafundisho ya Biblia:
Kuwa Mtu Mkweli

4

Sheria ya Kutaka Tuwe
Watu Wakweli

5-6

Maswali na Majibu

7

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa
Msimu Huu

8

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

butwaa na hali ya kujirudia, vijana wakafunga mwili wa Anania wakauchukua na kuuzika siku hiyo kwa kulingana na tamaduni za kale za Wayahudi.

Lakini masaa matatu baadaye Safira akafika katika mkutano huo bila kujua kilichokuwa kimeendelea. Mtume Petro akamkaribia na kumuuliza, “Mliuza kiwanja kwa thamani hiyo?” Safira akamjibu, “Ndio.” Naye Petro



“Kama hukumu ya Mungu ingewaangukia waongo na wanafiki wote walioko katika makusanyiko ya kanisa katika siku hizi zetu, ni nani kati yetu angeliokoka?”

akamwambia, “Imekuwaje hata mkapatana kumjaribu Roho wa Bwana? Angalia, miguu yao waliomzika mumeo ipo mlangoni, nao watakuchukua nje wewe nawe.”

Mara moja Safira akaanguka chini akafa. Nao vijana waliokuwa wamemzika mumewe wakaingia na kuuchukua mwili wake kwenda kuuzika kando kando ya mumewe. Hukumu ya Mungu dhidi ya Safira ikawa sawia na ile ya mumewe. Yeye alikuwa mshiriki katika dhambi ya kuhadaa, nayo hukumu ya Mungu haikupungua.

Maandiko yanatilia mkazo kwamba hofu ilitandaa kati ya watu wote kutokana na tukio hilo, “Hofu nyingi ikawapata kanisa lote na watu wote walioyasikia haya.” Hebu woga wa Mungu uwaingie watu wote walioko ndani na nje ya kanisa. Huenda watu walianza kuchunguza maisha yao na kuanza kuogopa kusema,

kutenda, au kuishi katika njia za udanganyifu. Hata ingawa watu huwa na hisia nyingi jambo kama hilo likitokea, hisia hizo huwa sio za kudumu, muda si muda wao hurudia tabia zao za kawaida.

Kama hukumu ya Mungu ingewaangukia waongo na wanafiki wote walioko katika makusanyiko ya kanisa katika siku hizi zetu, ni nani kati yetu angeliokoka? Wengi wa watu wanaojiita Wakristo wanaishi maisha ya kuhadaa wale wengine na hawawi wakweli katika mahusiano yao na Mungu, kwao binafsi, na kwa watu wale wengine. Ni kweli kwamba Anania na Safira walitoa sadaka kubwa, lakini sadaka hiyo haikuwa kubwa kushinda udanganyifu wao. Mtu kuwa na imani ya kweli na pia kufanya matendo mema sio mambo ambayo yanaweza kumwondolea lawama au kumfanya ahesabiwe haki anaposema uongo.

Mwisho kabisa hukumu ya Mungu itaingia; kifo cha milele kinawasubiri wale ambao wanasema uongo na kukosa kutubu dhambi hizo zao. Je, wewe utaepukana na hukumu hiyo?

Wewe mwongo! Tahadhari! ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

Tahariri



Tuombeeni; maana tunaamini kwamba tuna dhamiri njema, tukitaka kuwa na mwenendo mwema katika mambo yote. —Waebrania 13:18

Ombi la mtume Paulo lilikuwa kwamba wao wawe na dhamiri njema na kuwa wakweli katika mambo yote. Ni ombi langu kwamba Bwana atawahakikishia watu wote ambao wana shauku la kumtumikia umuhimu wa kuishi katika ukweli wa mambo kila siku. Tumeitwa ili tuishi maisha ya utakatifu bila kuwa na hadaa zozote.

Somo la robo hii ya mwaka linahusiana na haja ya sisi kuwa wakweli. Hata ingawa hili ni somo la kimsingi katika Ukristo, ni somo ambalo pia ni muhimu. Ni jambo la huzuni kwamba wengi wanaojiita Wakristo hudanganyana, huibiana, husema uongo, na hata kuhadaa wale wengine. Hadithi zinazohusu watu ambao hawaishi katika ukweli zimejaa katika fani za kisiasa, michezo, biashara n.k., na upotovu huo ndio umeharibu maisha ya mahusiano katika jamii nyingi. Lakini hata ingawa jambo hilo ni la kawaida katika ulimwengu wa dhambi, kamwe hili silo jambo ambalo linahitaji kusikika kati ya watu wa Mungu. Haja ya sisi kuwa wakweli na kuwa na mwenendo mwema “katika mambo yote” ni jambo la kimsingi la mfuasi wa Yesu Kristo.

Ni jambo la kushangaza jinsi watu wanaweza kutoa visingizio na vijisababu vya kuwahadaa wenzao na wao kutokuwa wakweli, mradi mambo wanayofanya inawafaidi—iwe ni habari wanayoambia watoto wao, shughuli zao za kibiashara, mawasiliano katika ndoa, yale ambayo watoto wanawaambia wazazi, na hata katika shughuli za kujaza fomu za kulipa ushuru. Lakini uongo mmoja tu ndio utasababisha wewe ukose Mbinguni. Wewe hutakosa kufika mbinguni kwa sababu ya msururu wa kusema uongo, bali ni kutokana na neno moja la uongo. Ni bora zaidi mtu kukubali upungufu wake, kukubali kwamba yeye sio mkamilifu, au kwamba amepungukiwa na hekima, badala ya kusema uongo ili kuepuka majukumu yake. Kusema kweli wengi wetu wameahidi kufanya jambo fulani na papo hapo tukasahau ahadi yetu. Hata ingawa jambo hilo sio dhambi, kwa sababu limetendwa bila kukusudia, kuna haja ya sisi kuwa waangalifu katika maneno tunayosema kutoka kinywani mwetu. Wakati mtoto wa Mungu amekuahidi kufanya jambo fulani, unahitaji kutarajia kwamba yeye atafanya hivyo. Lakini Wakristo wengi wameanza kutotilia maanani maneno yao na kutowajibika kwa yale wanayosema, na jambo hili sio ushuhuda mzuri kwa ulimwengu.

Ni baraka kubwa mtu kuishi maisha ya ukweli. Hata ingawa sisi wakati mwingine tutafanya makosa, tutapungukiwa kama wanadamu, na hata wakati mwingine tutasahau mambo tuliyoahidi watu wengine, kuna amani kubwa inayopatikana kutokana na mtu kuishi maisha ya ukweli. Hebu basi kila msomi wangu apate changamoto ya kuendelea kuishi maisha ya kweli na ya uadilifu.

Michael W. Smith

Januari, 2022

KISA CHA ZIZI LA NG'OMBE

Mimi ninamfahamu mtu mmoja ambaye alikuwa akifanya kazi ya kuwatunza mayatima waliokuwa maskini. Watoto hawa walilala sakafuni ambako kulikuwa na uchafu mwingi na wakawa na mahitaji mengi maishani. Mimi nami nilikuwa na moyo wa kuwasaidia watoto hao, lakini hekima ikaniambia kwamba nilihitaji kwanza kuhakikisha kwamba mtunzaji huyo angeweza kuaminika na hazina kidogo. Basi siku moja nikapata pesa ambazo zingemwezesha kununua ng'ombe ambayo ingewapatia watoto hao maziwa ya kunywa. Ng'ombe huyo naye alihitaji zizi la kumkinga dhidi ya makali ya hali ya hewa, na pia kumkinga dhidi ya kuchomwa na jua. Basi kulingana na bajeti

ya mtu huyo mimi nikamwachia pesa nyingi za kujenga zizi nzuri la ng'ombe. Lakini niliporudi na kumtembelea nikatazama ili niweze kuona zizi hilo la ng'ombe. Lakini kamwe mle hamukuwa na zizi la ng'ombe.

“Mbona wewe hunisaidii?” ni swali ambalo huulizwa na watu wengi: “Je, zizi la ng'ombe liko wapi?”

Kama ambavyo Yesu alisema katika Luka 16:10, “Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia.”



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujiandikisha na

kupata jarida

za mbele.



Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: Kuwa Mtu Mkweli

Somo la Maandiko: *Midomo ya uongo ni chukizo kwa BWANA; Bali watendao uaminifu ndio furaha yake.* —Mithali 12:22

Maelezo: Mtu mkweli ameelezwa “Kuwa mtu asiye na hadaa; mwenye kusema ukweli, mtu mwaminifu . . . mwenye kufuata maadili bora, au mwenye kufuata mambo yanayofaa” (*Kamusi ya Oxford*). Hali ya mtu kuwa mkweli ni kuwa mtu anayeaminika, “Mwenye kujizuia kusema uongo, kunyang’anya, au kuiba” (*Kamusi ya Collins*).

Muhstasari: Sifa ya asili ya Mungu ni ya utakatifu na ukweli; Yeye huchukia uongo wa aina yote. Wakristo wanahitaji kuwa wakweli katika fani zote za maisha yao—kwa maneno na matendo. Kukosa kuwa mtu mkweli ni kukosa kufuata maadili bora na tabia za ukweli, na matokeo yake ni mtu kupata hukumu ya milele.

I. Mungu wa Kweli

- A. Kumbukumbu 32:4 Mungu ni Mwadilifu.
- B. Waebrania 6:18 Mungu hawezi kusema uongo.
- C. Tito 1:2 Mungu asiyeweza kusema uongo.

II. Chanzo cha Ukosefu wa Ukweli

- A. Yohana 8:44 Ibilisi ni baba wa uongo.
- B. Yereimia 9:5-6 Watu wanauzoesha ulimi wao kusema uongo.

III. Mungu Anachukia Uongo

- A. Mithali 6:16-17 Bwana achukia ulimi wa uongo.
- B. Zaburi 101:7 Asemaye uongo hatakaa nyumba yangu.
- C. Mithali 21:3 Kutenda haki hupendeza kuliko sadaka.

IV. Amri ya Kutosema Uongo

- A. Walawi 19:11-13 Msiibe, wala msidanganye, wala msiambiane uongo.
- B. Wakolosai 3:9 Msiambiane uongo.

V. Shahidi Mwongo

- A. Kutoka 20:16 Usimshuhudie jirani yako uongo.
- B. Mithali 12:17 Atamkaye maneno ya kweli hufunua haki.

VI. Sema Ukweli

- A. Zaburi 34:13 Midomo isiseme hila.
- B. Waefeso 4:25 Vueni uongo, mkaseme kweli.

VII. Msiape, Msiahidi

- A. Mathayo 5:37 Maneno yenu yawe ndiyo, ndiyo.
- B. Yakobo 5:12 Msiape.

VIII. Kuwa Mkweli kwa Mungu na Kwako Binafsi

- A. Zaburi 15:1-3 Asemaye kweli kwa moyo wake.
- B. 1 Yohana 1:6 Kusema yasiyo ya kweli ni kusema uongo.
- C. Wafilipi 4:8-9 Tuseme mambo yaliyo ya kweli na haki.

IX. Mwongozo wa Kuwa Mtu Mkweli

- A. 2 Wakorintho 8:21 Kufikiri yaliyo mema.
- B. 2 Wakorintho 4:2 Kukataa mambo ya aibu na hila.
- C. Matendo 24:16 Dhamiri isiyo na hatia.
- D. 1 Petro 2:21-22 Mfano wa Kristo—mkosefu wa hila.

X. Viongozi Wanatakiwa Kuwa Wakweli

- A. Kutoka 18:21 Chagueni watu wa kweli.
- B. Matendo 6:3 Chagueni watu walioshuhudiwa kuwa wema.

XI. Kudanganya/Biashara/Ulipaji Ushuru

- A. Mithali 11:1 Mizani ya hadaa ni chukizo.
- B. Yereimia 22:13 Nyumba ijengwayo kwa uovu.
- C. Ezekieli 22:13 Faida isiyo ya haki.
- D. Warumi 13:7-8 Lipa ushuru. Msidaiwe na mtu.

XII. Gharama ya Kuwa Mtu Mkweli

- A. Mithali 16:8 Afadhali mali kidogo pamoja na haki.
- B. 1 Petro 3:17 Kuteswa kwa kutenda mema.
- C. Zaburi 15:4 Ameapa kwa hasara yake.

XIII. Faida na Baraka za Ukweli

- A. Yohana 8:32 Kweli itawaweka huru.
- B. Mithali 12:19 Utadhibitishwa milele.
- C. 1 Petro 3:10 Kuona siku njema.
- D. Mithali 16:13 Furaha ya wafalme.
- E. Zaburi 145:18 Bwana yu karibu.

XIV. Matokeo ya Kutokuwa Mkweli

- A. Luka 12:2 Maneno yote yatafunuliwa.
- B. Mithali 19:5 Shahidi wa uongo hakosi ataadhibiwa.
- C. Ufunuo 21:8 Waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti.

Tamati

Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu. —Warumi 13:13

SHERIA YA KUTAKA TUWE WATU WAKWELI

Jamii za watu zinafanya juu chini kutoa maana tofauti kwa mambo yanayofaa na yasiyofaa, na kusema kwamba hakuna mambo ambayo Muumbaji amesema yanafaa au hayafai. Lakini hata ingawa uovu umezidi kila mahali na watu wanajaribu kupima mambo ambayo yanafaa kwa kutumia akili zao, Mungu ana kanuni ambazo Yeye hutumia kuhukumu ulimwengu.



“Uongo—ambao maana yake ni mtu kusema kisicho cha kweli kwa makusudi ili kumhadaa mwenzake—ni jambo linalotokana na dhambi.”

Mungu ni mtakatifu, msafi, na mkweli, na pia ni “Mungu wa uaminifu, asiye na uovu” (Kumbukumbu 32:4). Kwa kweli “Mungu hawezi kusema uongo” (Waebrania 6:18). Ukosefu wa ukweli ni jambo ambalo liko kinyume na sifa zake Mungu, kwa maana Yeye ni mkamilifu na ni Mkweli kabisa.

Chanzo cha Ukosefu wa Ukweli

Watu kusema uongo na kuhadaa wenzao ni jambo la kawaida. Lakini kulingana na Kristo, Shetani ndiye baba wa uovu wote na kuzorota kwa tabia za wanadamu. “Ninyi ni wa baba yenu . . . kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. . . kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo uwongo” (Yohana 8:44). Uwongo wote na ukosefu wa ukweli ni mambo yanayotokana na Ibilisi. Yeremia 9:5-6 inasema kuhusu watu waliomuacha Mungu na kuhadaa majrirani zao, na “wameuzoeza ulimi wao kusema uongo.” Moyo ambao sio safi na nguvu za kimwili ambazo zinaongozwa na Shetani ndizo humfanya mtu kusema uwongo.

Mungu wa Ukweli

Katika Sheria ya Musa maana ya dhambi imeelezwa kinaga ubaga, na kuonyeshwa kwa njia dhahiri, lakini pia mambo hayo yakaandikwa katika dhamiri za watu wakati ambapo ulimwengu uliumbwa, ili kwamba dhamira zetu ziweze kutushuhudia kuhusu sheria za Mungu, sheria za maumbile ya ulimwengu. Kuweza kuaminika na kuwa mtu mkweli ni mambo ya kimsingi katika sheria za maumbile hayo na ambazo zilizinduliwa na Mungu mwenyewe. Ukosefu wa ukweli (kwa njia ya watu kuwa waongo, wadanganyifu, wezi) ni mambo ambayo yako kinyume kabisa na mpango na matakwa yake Mungu katika maisha ya Mkristo.

Amri ya Kutosema Uwongo

Ulimi wa kusema uwongo ni moja ya mambo sita ambayo Mithali 6:16 inasema Mungu huchukia. Hakuna haja ya Mkristo kusema uwongo, hata ikiwa ni uongo mdogo kiasi gani. “Hatakaa ndani ya nyumba yangu mtu atendaye hila. Asemaye uongo hatathibitika mbele ya macho yangu” (Zaburi 101:7). Masomo yote makuu ya kithiolojia, mafundisho makuu ya kidini, au jitihada za kutenda matendo mema sio sababu tosha za kufanya mtu asiwe mkweli, kwa sababu “Kutenda haki . . . humpendeza BWANA kuliko kutoa sadaka” (Mithali 21:3).

Amri za Agano la Kale ni dhahiri: “Msiibe, wala msidanganye, wala msiambiane uongo . . . usimdhulumu jirani yako” (Walawi 19:11-13). Vile vile “Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake” (Wakolosai 3:9). Uongo—ambao maana yake ni mtu kusema kisicho cha kweli kwa makusudi ili kumhadaa mwenzake—ni jambo linalotokana na dhambi. Naye mtoto wa Mungu hatakiwi tena kuishi au kusema mambo kutoka kwa moyo au ulimi mdanganyifu.

Sema Ukweli

Moja ya Amri Kumi za Mungu inasema kwamba, “Usimshuhudie jirani yako uongo” (Kutoka 20:16). Kusema mambo kuhusu mtu mwingine ambayo si ya kweli ni kuvunja sheria ya kimsingi ya Mungu. Ni mtu kukosa kudumisha maadili yanayokubalika. Matendo na maneno ya Mkristo yanahitaji kuwa ya kweli na ya kuaminika. “Uuzuie ulimi wako na mabaya, na midomo yako na kusema hila” (Zaburi 34:13). Naye mtume Paulo akawaambia watu wa Efeso waweke kando uwongo wote na badala yake wanene ukweli (Waefeso 4:25).

Msiape, Msitoe Ahadi

Watu wengi hutumia usemi kwamba, “Naapa kwamba . . .” au “Natoa ahadi kwamba . . .” Basi kama Mkristo haapi au kutoa ahadi kwa yale anayosema hii ni kusema kwamba yeye sio mkweli kwa anayosema au kwamba anasema uongo? Maandiko yamemwamuru Wakristo “msiape, wala kwa mbingu wala kwa nchi; wala kwa kiapo kinginecho chote; bali ndiyo yenu na iwe ndiyo, na siyo yenu iwe siyo” (Yakobo 5:12). Naye Yesu aliwafundisha

(Endelea katika Ukurasa 6)

watu “maneno yenu yawe Ndiyo, ndiyo; Siyo, siyo; kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu” (Mathayo 5:37). Kwa usemi mwingine Mkristo hana haja ya kuapa au kutoa ahadi kuhusu jambo fulani. Kama Mkristo atasema jambo, jambo analosema linahitaji kuwa kweli, lenye kuaminika, lisilo danganyifu. Tabia zetu za kutoa ahadi ndizo hudhoofisha ukweli wa mambo mengine ambayo tunasema lakini hatuyatolei ahadi.



Wakristo wanastahili kuwa na uhusiano wa kweli na watu wote, bila kujali umri au cheo. “Tukitangulia kufikiri yaliyo mema, si mbele za Bwana tu, ila na mbele ya wanadamu” (2 Wakorintho 8:21). Katika 2 Wakorintho 4:2 mtume Paulo anasema kuhusu Wakristo kwamba “tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila.” Sio kwa matendo na maneno peke yake, bali makusudi na malengo yetu yote yanahitaji kuwa ya kweli. Kristo alituachia mfano wa kufuata. Hakukuwa na udanganyifu au hadaa mdomoni pake (1 Petro 2:21-22). Yeye alikuwa mkweli, na akasema ukweli, na pia alikuwa mtu mwenye kuaminika. Kila Mkristo anahitaji kuwa kama mtume Paulo ili adumishe “dhamiri isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele ya watu siku zote” (Matendo 24:16).

“Mtu kuwa mkweli katika nafsi yake mwenyewe, na kwa Mungu, ndio njia ya pekee ya kuweza kukua kiroho na kujiandaa ili kukutana na hukumu itakayokuja.”

Ukweli Mbele Zake Mungu na Mtu Binafsi

Ni jambo muhimu sana mtu kuwa mkweli mbele zake Mungu na kwa dhamiri yake. Daudi alimuuliza Mungu, “ni nani atakayekaa katika hema yako?” Moja ya jibu lake lilikuwa kwamba: “Asemaye kweli kwa moyo wake” (Zaburi 15:1-3). Watu wengine hujiambiwa uwongo mwingi hivi kwamba wao huanza kuamini uongo huo na kuanza kuishi maisha ambayo si yao. Lakini hili ni jambo ambalo halitafaidi afya yako, na pia ni jambo ambalo halifai. Mkristo anahitaji kutafakari kuhusu mambo yaliyo ya kweli, yaliyo ya haki, yenye sifa njema (Wafilipi 4:8-9). Zaidi ya hayo 1 Yohana 1:6 inasema kwamba, “Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli.” Mungu anachukia unafiki wa aina zote, na kila mmoja wetu anahitaji kuwa mkweli katika nafsi yake kiakili na kiroho. Mtu kuwa mkweli katika nafsi yake mwenyewe, na kwa Mungu, ndio njia ya pekee ya kuweza kukua kiroho na kujiandaa ili kukutana na hukumu itakayokuja.

Viongozi Wanatakiwa Kuwa Wakweli

Kama ambavyo Wakristo wanatakiwa kuwa wakweli, viongozi wa kanisa nao wanatakiwa kuwa wamehitimu katika swala hili la kuwa watu wakweli. Wale viongozi wa wana wa Israeli walitakiwa kuwa “watu wa kweli” (Kutoka 18:21), nao mashemasi ambao walichaguliwa katika Matendo 6:3 walihitaji kuwa “walioshuhudiwa kuwa wema.”

Kuhadaa Katika Biashara na Ulipaji Ushuru

Wakristo wanatakiwa kuwa wakweli kwa mambo yote; nyumbani, shuleni, katika biashara zao, katika kutimiza matakwa ya kiserikali, n.k. Udanganyifu ndio mahali ambapo wizi na kusema uwongo zinakutana. Nabii Yereimia alisema kuhusu watu wenye kujenga nyumba yake kwa hadaa na kukosa kulipa wafanyi kazi wake mishahara yao (Yereimia 22:13). “Mizani ya hadaa ni chukizo kwa Bwana; bali vipimo vilivyo sawasawa humpendeza” (Mithali 11:1). Wakristo wakweli watalipa madeni yao, watafanya kazi yao wenyewe, watakuwa wakweli katika shughuli zao zote za kibiashara, na kwa hiari hawawezi kumnyang’anya mtu yeyote iwe kwa jambo kubwa au ndogo. Katika kuishi maisha ya ukweli, Mkristo atatoa ripoti za kweli na kulipa ushuru wote ambao anastahili kulipa kwa serikali (Warumi 13:7-8). Wakati Mkristo amesema jambo, jambo hilo linastahili kuchukuliwa kuwa la kweli na linalofaa, na matendo yake yanahitaji kulingana na aliyosema. Jambo lote ambalo halitokani na ukweli ni dhambi.

Gharama ya Kuwa Mtu Mkweli

Kuna nyakati ambapo itakugharimu wakati na mali yako ili kudumisha ukweli wako, lakini jambo hili linampendeza Mungu. Zaburi 15:4 inasema kuhusu mtu ambaye “Ingawa ameapa kwa hasara yake, hayabadili maneno yake.” Wakati umesema utafanya jambo fulani, wewe tenda hilo hata ingawa utaumia. Walimwengu hubadilika na kurudi nyuma kwa maneno yao, lakini mtoto wa Mungu huishi kwa uaminifu. Ni bora kuishi kwa kidogo na haki (Mithali 16:8) na kuwa na baraka zake Mungu.

Baraka Zinazoletwa na Maisha ya Ukweli

Uaminifu na kuishi maisha ya ukweli ni mambo ambayo humweka mtu huru kwa sababu “kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru” (Yohana 8:32). Uongo huja na kwenda lakini ukweli ndio hudumu (Mithali 12:19), na mtu mkweli kamwe hawi na uwoga wa kushikwa akisema uwongo. Wasemao ukweli wanaheshimiwa na kupewa vyeo (Mithali 16:13). Siku za furaha huja kwa wale wasemao bila kusema uwongo na hadaa (1 Petro 3:10). Na jambo kuu zaidi ni kwamba, “Bwana yu karibu na wote wamwitao, wote wamwitao kwa uaminifu” (Zaburi 145:18).

Matokeo ya Mtu Kutokuwa Mkweli

Hakuna jambo lolote linalotendeka au kusemwa maishani haya ambalo milele litakuwa siri, hata ikiwa wanadamu watandanganywa kwa muda kidogo. Mambo yote yatakuwa wazi (Luka 12:2), na hakuna shahidi mwongo au mtu mwenye kusema uongo ambaye ataepuka hukumu yake Mungu (Mithali 19:5). Kwa mtoto wa Mungu maisha ya ukweli si jambo la kujichagulia au kutojichagulia, ni jambo la lazima kwa Mungu. Wale wanaosema uongo watapata adhabu ile ile kama ya wale ambao hawaamini Injili na kama wauaji. “na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti” (Ufunuo 21:8).

Basi hebu tuishi, tuwaze, tunene, na kutendo mambo yote kwa ukweli kama ambavyo tumeamriwa na Neno la Mungu, bila kuwa na uwongo wowote, hadaa yoyote, au kukuwa watu wasio na ukweli. ■



“Biblia haifundishi maadili ambayo yanategemea hali ambazo tunajipata ndani mwake. Ukweli wa Mungu haupingiki, na kusema uwongo ni ishara ya tabia na utu ambao sio mkamilifu.”

Je, kuna wakati ambapo imekubalika mtu kusema uwongo ili kuleta mema zaidi?

Kwa mawazo ya kilimwengu pengine kuna hali ambazo zinaweza kujadiliwa ambazo kunaweza kuonekana vizuri kusema uwongo. Lakini Biblia inasema wazi. 1 Petro 3:10 inafundisha kwamba midomo yetu isiseme mambo ya hila. Hii ni kumaanisha kwamba chochote tusemacho kinahitaji kuwa cha kweli, na tunahitaji kujikinga dhidi ya kuwaharibia watu majina kwa kuwasema mabaya, tusiwe waongo, tusiwe watu wadanganyifu, na tusiwe watu wenye hadaa. Amri hii haitegemei hali ambazo sisi tunajipata.

Biblia haifundishi maadili ambayo yanategemea hali ambazo tunajipata ndani mwake. Ukweli wa Mungu haupingiki, na kusema uwongo ni ishara ya tabia na utu ambao sio mkamilifu. Wakati mmoja binti yangu aliniuliza kama ninaweza kuingiza Biblia kwa njia ya magendo kwa nchi ambayo imepiga marufuku jambo hilo. Kwa kweli mimi naweza kuvunja sheria ya mwanadamu na kuwapatia watu wa nchi hiyo Biblia. Na kamwe siwezi kwa hiari yangu kutoa habari kwa serikali hiyo kuhusu kile ninachofanya; lakini ikiwa wenye mamlaka wataniuliza swali la moja kwa moja kuhusu jambo hilo, kamwe mimi sitokana ukweli, hata kama nitatupwa korokoroni.

Kusema uwongo na kudanganya ni kinyume cha yote ambayo ni mema na yanayofaa. Wakati kama huo inaweza kuonekana kama ni jambo bora litatendeka kutokana na usemaji wa uwongo, lakini mwishowe tendo hilo la kusema uwongo litaleta maangamizi makubwa. Matokeo mambo ya wokovu ni mtu kupata urembo unaingia maishani mwake—anakuwa mtu sawa kote kabisa. Lakini ukiingiza uwongo maishani hayo, basi utapata umechafuka na inakuwa sasa wewe sio safi kabisa.

Je, unaweza kutoa mawaidha gani kwa wazazi kuhusiana na swala la wao kuwa wakweli kwa watoto wao?

Kwanza kabisa wazazi wanahitaji kuwaambia watoto wao ukweli kila wakati. Hata ingawa si busura mzazi kumwambia mtoto kila kitu anachotaka kujua, madhara yaletwayo na kumwambia mtoto uwongo huwa makubwa zaidi. Wazazi wengine hutoa ahadi kwa watoto halafu wanakosa kutimiza ahadi hizo. Jambo hili linawafundisha watoto kwamba ni sawa kusema kitu wakati fulani bila

kuwajibika kulitimiza jambo hilo. Ikiwa mzazi atamwambia mtoto kwamba watatembea mahali fulani, au watafanya jambo fulani, mzazi huyo anahitaji kuwa na uhakika kwamba atatimiza aliyoahidi. Watoto hujifunza zaidi kwa kutazama mambo yanayofanyika machoni pao na kwa ujuzi wanaopata maishani kuliko yale ambayo tunawaambia.

Pili, wazazi wanahitaji kufunza watoto wao umuhimu wa wao kuwa wakweli huku wakiwa wangali na umri mdogo. Wakifikisha miaka miwili au mitatu watoto huwa na uwezo wa kusema uwongo, hasa kwa kukana wanapofanya makosa. Na wanapofikisha miaka minne watoto hao huwa na uwezo wa kutofautisha ukweli na uwongo, na wakati mwingi wao hujaribu kuficha makosa yao. Tabia hii ya kusema uwongo inaweza kukua ndani ya mtoto ikiwa haitarekebishwa mapema. Kuna utafiti unaosema kwamba asilia 96 ya watoto wachanga hufanya jitihada za kuficha makosa yao. Wengi wao hudanganya mara nyingi kwa siku.

Basi ni jambo muhimu wazazi kuwafunza watoto wao kusema ukweli na kuwataka wawe wakweli wanapojua kwamba mtoto anajaribu kuwa mwongo. Tendo la mtoto kusema uwongo sio tendo la kufurahisha mzazi. Wao wanahitaji kupewa nidhamu na tabia hiyo inahitaji kurekebishwa mara moja kwa kuwapatia matokeo ya tabia yao, iwe ni ya kupendeza au ya uchungu, ili watoto hao wajifunze umuhimu wa wao kuwa wakweli.

Kuna mtu aliniuliza swali, na mara moja nikampatia jibu ambalo halikuwa la kweli. Je, nilitenda dhambi?

Kusema uwongo ni jambo ambalo hufanyika wakati mtu amesema jambo makusudi kwa ajili ya kumpotosha mwenzake. Kama hukuwa na wakati wa kufikiria jambo hilo, na jambo la kwanza lililokuja akilini ni kutoa jibu “la kuingia maslahi yako” na baadaye ukagundua huo haukuwa ukweli, hapo hujatenda dhambi. Lakini ni muhimu wewe kurudi kwa mtu huyo na kurekebisha maneno yako, hata ingawa utalionea aibu jambo hilo. Kuna masomo utapata na onyo ulimini mwako kutokana na tendo hilo la kurudi kwa yule uliambia uwongo na kufanya marekebisha. Lakini ikiwa mtu amesema jambo kwa kusudi la kuhadaa mwenzake, mtu kama huyo hatakuwa tayari kurudi ili kurekebisha jambo hilo, kwa maana moyo wake umejaa hadaa. Wakati kama huo kuna haja ya mwenye kufanya makosa kutubu, ndio aweze kuokoka.



JE, WAJUA?

Asilimia 76% ya watu wanaamini kwamba kusema uwongo ni jambo ambalo linakubalika kwa baadhi ya nyakati.

Asilimia 24.1% ya wanaume washawahi kusema uwongo katika kujieleza kibinafsi katika facebook, huku asilimia ya wanawake ambao wamesema uwongo huo wakiwa ni 16.3%.

Asilimia 24.1% ya wanaume washawahi kusema uwongo wakijaza makaratasi yao ya kuomba kazi, ilhali asilimia ya wanawake ni 16.3%.

Asilimia 51.7% ya wanawake washawahi kusema uwongo kuhusu kipimo cha uzito wa miili yao, ilhali asilimia ya wanaume ni 28%.

Asilia 3% ya Wamerakani ambao walishiriki katika utafiti huu (kwa jumla watu 1,254) walisema kwamba wakati mwingi wao huongea uongo.

Lakini asilimia 66% yao walisema kwamba wakati mwingi wao huwa ni wakweli na hata wengine wakasema kamwe hawasemi uwongo.

Ni rahisi zaidi wanawake kudanganya wazazi wao ilhali wanaume angalau huhadaa marafiki zao.

(Utafiti uliofanyika nchini Marekani mwaka 2014, ambao ulifanywa kwa kutumia CreditDonkey.com).



CHUNGU KISICHO NA KITU

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

(Muhstasari wa hadithi ya kale ya Uchina. Ambayo kwanza ilirekodiwa na Demi.)

Kuna hadithi ambayo huhadithiwa katika nchi ya Uchina ya mvulana mmoja aliyejulikana kama Pingi. Yeye alipenda sana maua na chochote alichopanda kiliweza kukua na kuwa maua yenye urembo. Katika ufalme ambao Pingi aliishi mfalme huyo hakuwa na mwana, na alihitaji mtu wa kuchukua mahali pake. Mfalme huyo ambaye pia alipenda kazi ya kulima aliwapatia wavulana wa ufalme huo mbegu za kupanda maua. Yule mvulana ambaye angeweza kukuza maua marembo zaidi ndiye angechukua mahali pake na kuwa mfalme. Basi Pingi akapanda mbegu hiyo ya mfalme kwa uangalifu mkubwa katika chungu kilichokuwa na mchanga wenye rutuba. Akaitunza na kuihifadhi vizuri mbegu hiyo kwenye mchanga, lakini hakuna chochote kilimea.



Wavulana wale wengine nao wakapanda mbegu zao na kupata maua mazuri yakimea katika vyungu vyao. Ndiposa wakamchekelea na kumdhihaki Pingi ambaye alikuwa ndiye pekee alikuwa na chungu ambacho ndani yake hakukuwa na chochote kilichokuwa kikimea. Basi Pingi akabadilisha mchanga na kuweka mbolea ya samaki waliokauka, lakini juhudi zake hazikufua dafu. Basi mwishowe siku ikafika ambapo mimea hiyo ingepeleka kwa mfalme. Huku wavulana wengine wakiwa na furaha kubwa, Pingi mwenyewe alikuwa amekufa moyo na kukata tamaa, kwa maana mle chunguni mwake hamkuwa na chochote. Lakini baba yake akamkumbusha kwamba yeye alikuwa amefanya jitihada zote na basi kilichobaki ni kumpelekea mfalme chungu hicho kisichokuwa na kitu.

Watoto hao wa ufalme wakafika katika makao ya mfalme huku wakiwa na maua yao yenye urembo. Mfalme naye akachunguza mimea ya wavulana wao huku akikunjamana uso wake. Uso huo ulizidi kukunjamana zaidi alipoona chungu cha Pingi ambacho hakikuwa na chochote mle. Naye kamfokea, "Umeniletea chungu kisicho na kitu!" Pingi naye akainamisha uso wake kwa aibu na kumwambia mfalme, "Niwie radhi Mfalme. Mimi nilijaribu kukuza hiyo mbegu ambayo ulinipatia, lakini hakuna chochote kilimea."

Mfalme naye akaguza kidevu chake na kutabasamu. Halafu akawaambia watu wa ufalme wake, "Hebu niwajulishe kwa mfalme wenu mpya. Hizo mbegu zilikuwa zimepikwa, kwa hivyo kamwe hazingeweza kumea. Mimi sijui nyinyi wengine mlikuza mimea yenu kwa njia gani, lakini hizo maua zenu hazikumea kutokana na mbegu nilizowapatia. Kijana huyu Pingi ni mkweli na ni mwenye roho ya kifalme." ■